Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 06 -9
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412
Telephone +44 (0) 1604 463578

9781902059068

Facsimile +44 (0) 1604 765068
Email: CarlHinton@hotmail.com
Web: http:\\go.to\Carl_Hinton

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 12-15

Correspondence Course Lessons 12-15

Tena:

1 902059 00 - X	Matayarisho ya Ubatizo
1 902059 01 - 8	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 1-4
1 902059 02 - 6	Ukimwi
1 902059 03 - 4	Mshitaki Wenu Ibilisi
1 902059 04 - 2	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 5-8
1 902059 05 - 0	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 9-11
1 902059 06 - 9	**Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 12-15**
1 902059 07 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 16-19
1 902059 08 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 20-23
1 902059 09 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 24-27
1 902059 10 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 28-31
1 902059 11 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 32-36
1 902059 12 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 37-40
1 902059 13 - 1	Ufunuo mlango wa kwanza - Maelezo ya maneno ya mstari kwa mstari

14c Kazi ya ziada
Andika habari fupo kuhusu Yerusalemu: (a) Katika wakati uliopita; (b) Wakati wa sasa; (c) Kwa wakati ujao. (Masomo 9 na 14, na kusoma kwako Biblia kutakusaidia.)

15a (a) Mungu anamwahidi nini Mfalme Daudi?
(b) Ni "Mwana" yupi muhimu katika ahadi hizi?
(c) "Mwana" huyu atatawala kutokea kiti cha enzi cha Daudi. Kiti cha enzi cha Daudi kilikuwa wapi?
(d) Andika Matendo ya Mitume 13:23. Elezea mstari huu una maana gani?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO
Na. 12.

AHADI ZA MUNGU KWA ABRAHAMU

Kusoma: Mwanzo 13



Karibu miaka 2000 kabla ya kuzaliwa Yesu, kulikuwa na mtu aliye ishi aliyeitwa jina lake Abramu, aliyesemwa katika Biblia kuwa ni rafiki ya Mungu (Isaya 41:8). Aliishi katika mji wa Uru, ambao upo katika nchi inayo itwa sasa Iraq, karibu maili 800 mashariki ya nchi ya Israeli. Watu wa Uru hawakujua chochote kuhusu Mungu wa kweli Waliabudu miungu mingi ya uongo, mungu wao mkubwa alikuwa ni mwezi. Magofu ya hekalu walilolijenga kwa mungu-mwezi yamepatikana kule.

Ujumbe toka kwa Mungu

Siku moja Abramu alipata ujumbe toka kwa Mwenyezi Mungu. Tunaweza kusoma ujumbe huu katika Mwanzo 12:1:

> *"BWANA akamwambia Abramu, utoke katika nchi yako, toka katika jamaa zako, na utoke katika nyumba ya baba yako, uende katika nchi nitakayo kuonyesha."*

Aliambiwa atoke kwenye nchi yake, na watu wake mwenyewe, na kusafiri katika nchi ambayo Mungu alimuonyesha. Inashangaza, tungejisikiaje kama tungepokea ujumbe kamahuu? (Kwa kweli kusafiri mbali ilikuwa ni matatizo zaidi na hatari sana katika siki hizo).

Wakati alipoambiwa kufanya hivi, Mungu alimwambia Abramu pia:

"Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe utakuwa baraka: nami nitawabariki wakubarikio, na kuwalaani wakulaanio: na atika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa" (mistari 2,3).

Abramu aliamini ahadi za Mungu alizozifanya, naye alimtii Yeye. Mwandishi aliye andika waraka kwa Waebrania anatuambia sisi kuwa Abrahamu *"alitoka, asijue alikokuwa anakwenda"(Waebrania 11:8).*
Mwisho alifika katika nchi ya Israeli pamoja na Sara mke wake, na mpwa wake, Loti. Sasa soma tena Mwanzo 13. Utaona jinsi Loti alivyo chagua nchi nzuri zaidi na Abramu aliachwa atafute malisho ya mifugo yake katika maeneo ya nchi kavu zaidi. Lakini Mungu alikuwa pamoja na Abramu, na aliongeza ahadi juu ya zile alizofanya naye Uru:

"Nchi yote unayo iona, nitakupa wewe, na uzao wako milele. Na nitaufanya uzao wako kuwa mwingi kama mavumbi ya nchi" (Mwanzo 13:15-16).

Ahadi ya ajabu

Umegundua kwamba wakati huu Mungu alimwahidi Abramu, baadaye aliitwa Abrahamu, nchi milele? Kumiliki nchi milele, Abrahamu itabidi aishi milele, hivyo Mungu alikuwa kweli anamwahidi uzima wa milele. Nchi aliyo ahidiwa ilikuwa ni nchi aliyo iona - nchi tunayo iita sasa Israeli.

Zaidi ya hivi, Mungu ali-iahidi nchi hiyo kwa uzao wa Abrahamu, au mwanawe. Wakati ule Abrahamu na Sara walikuwa hawana watoto. Mungu alimwahidi yeye 'uzao', au mwana, atakaye miliki pamoja naye hiyo nchi. Pia Abrahamu aliahidiwa kuwa wazao wake watakuja kuwa taifa kubwa.

Mungu afanya agano na Abrahamu

Geukia Mwanzo 15, na hapa utakuta kwamba Mungu tena anarudia na kuongeza ahadi zake kwa Abrahamu.

Muda ulipita na Abrahamu alianza kuzeeka. Mwana aliyeahidiwa hakupewa. Lakini maranyingine tena Mungu alimuhakikishia kuwa atakuwa na mtoto, na kwamba wazao wake wataku wa na idadi kubwa kama nyota za angani.

Katika mstari wa 6 tunasoma:

"Abrahamu alimwamini Bwana; Mungu alimuhesabia kwake ni haki."

Abrahamu, kama sisi, hakuwa huru toka dhambi; bali alimwamini Mungu na, kwasababu hii, Mungu alipendezwa naye. Wakati huu tunaambiwa kwamba Mungu alifanya naye agano - ambalo ni ahadi ya heshima ambayo kamwe haiwezi kubadilika. Utasoma namna agano hili lilivyofanywa katika Mwanzo 15:8-18.

masomo ya biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian.

Karatasi Ya Maswali Ya 4

Jaribu na ujibu maswali kwa maneno yako mwenyewe. Mahali panapotaja "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali ukipenda, au kuliacha kama utaona ni gumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali mengine yote. Kumbuka kuandika namba yako, jina na anuani yako juu ya kila karatasi ya majibu yako.

MASOMO 12 - 15

12a Mungu alimwambia Ibrahimu afanye nini wakati Ibrahimu alipokuwa akiishi Uru?

12b Mungu alimwambia Ibrahimu amfanye nini Isaka?

12c Neno "uzao" linamaanisha nini (kama ilivyo katika Mwanzo 13:15) ?

12d Ni uzao upi ulio muhimu sana wa Ibrahimu?

12e Kwa sababu Ibrahimu alimwamini Mungu na kumtii, Mungu alimbariki. Kati ya baraka zote hizo mbalimbali, zipi 2 unafikiri ni muhimu zaidi? Sema ni kwa nini.

13a Andika mistari michache kuhusiana na kila mojawapo ya majina yafuatayo: (a) Yusufu; (b) Musa; (c) Sauli.

13b (a) Kwa nini Mungu aliwafanya watu wa Israeli wachukuliwe uhamishoni?
(b) Ni katika nchi gani watu wa Yuda walipelekwa uhamishioni?
(c) Walikaa huko kwa muda gani?
(d) Walifanya nini mara baada ya kurudi?

14a Ni mistari ipi katika Zekaria 14 inalenga kwenye yafuatayo:
(a) Mataifa yote yatakuja kupigana na Yerusalemu.
(b) Bwana atawapigania Israeli.
(c) Yesu Kristo atarudi katika mlima wa Mizeituni.
(d) Bwana atakuwa Mfalme juu ya nchi yote.
(e) Watu waliofanya vita juu ya Yerusalemu watapigwa na tauni.
(f) Watu watakaosalia (wa mataifa yote waliokuja kupigana na Israeli) watakwea kwenda Yerusalemu kumwabudu Mfalme.

14b Katika maneno yako mwenyewe, yasiyozidi mistari 10, elezea unabii juu ya mifupa mikavu unamaanisha nini.

14c Kazi ya ziada

Andika habari fupo kuhusu Yerusalemu: (a) Katika wakati uliopita; (b) Wakati wa sasa; (c) Kwa wakati ujao. (Masomo 9 na 14, na kusoma kwako Biblia kutakusaidia.)

15a (a) Mungu anamwahidi nini Mfalme Daudi?
(b) Ni "Mwana" yupi muhimu katika ahadi hizi?
(c) "Mwana" huyu atatawala kutokea kiti cha enzi cha Daudi. Kiti cha enzi cha Daudi kilikuwa wapi?
(d) Andika Matendo ya Mitume 13:23. Elezea mstari huu una maana gani?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Katika kipindi cha Abrahamu, agano lilifanywa kwa kumchinja mnyama. Kisha mnyama aliyeuawa aligawanywa, na watu wawili wanao agana walitembea katikati ya vipande. Kwenye jambo hili, utukufu wa Mungu ulipita katikati ya vipande, kwasababu hiyo Abrahamu alijuwa kwamba agano lilikuwa ni lauhakika.

Mtoto aliye ahidiwa

Abrahamu alikuwa na miaka 100 na mke wake miaka 90, mwishowe Mungu alitimiza moja ya ahadi zake na akampa mtoto, ambaye walimwita Isaka.

Katika mwanzo 22 utaukuta mfano wa ajabu wa imani ya Abrahamu kwa Mungu. Soma mistari 14 ya kwanza. Mungu alimwambia Abrahamu amtoe mwanawe wa pekee Isaka, ili awe sadaka. Na hata hivyo Mungu alimwambia kwamba kwa kupitia Isaka wazao wa Abrahamu watakuwa taifa kubwa.

Abrahamu alifanya nini? Alijuwa kwamba Mungu atatunza ahadi zake, na hivyo mwandishi kwa Waebrania 11:17-19 anatuambia sisi namna hii:

> *"Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa, alimtoa Isaka: na yeye huyo alipokea ahadi (Abrahamu) alimtoa mwanawe wa pekee, kwa ambaye ilisemwa, "Yaani katika ISAKA uzao wako utaitwa": akahesabu kwamba Mungu aweza kumfufua toka wafu, toka huko tena akampata kwa mfano."*

Abrahamu alikuwa tayari hata kumtoa mwanawe mpendwa, akijuwa kwamba Mungu angemfufua. Sio ajabu Mungu alipendezwa na imani na utii. Soma Mwanzo 22:15 - 18 ahadi ambazo Mungu alizifanya tena kwake.

Uzao mkuu zaidi ya Isaka

Mambo haya yalitokea karibu miaka 4000 iliyo pita, na mara ya kwanza hayaonekani kwetu kuwa na maana sana. Bali Abrahamu alikuwa na mtoto mkuu kuliko Isako. Mstari wa kwanza wa Agani Jipya (Mathayo 1:1) unasema:

> *"Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu."*

Pia, Abrahamu aliahidiwa mtoto Yesu. Paulo anatuambia hili kwa Wagalatia 23:16:

> *"Sasa kwa Abrahamu na uzao wake ahadi zilifanywa. Hakusema, Na kwa wazao, kama a wengi; bali ya mmoja, Na kwa uzao wako, ambaye ni Kristo."*

Hivyo ahadi zilizofanywa kwa Abrahamu - ni kwamba ataishi milele kwenye nchi ya Israel na kuwa baraka kwa mataifa yote, na pia ahadi zililengwa kwa Bwana Yesu Kristo.

Yesu akirudi tena ili kutawala toka Yerusalem, tutaziona ahadi hizi kutimizwa.

Sisi, pia tunaweza kushiriki katika ahadi hizi

lkiwa tunamwamini Yesu, na kufanya anayo tutaka tufanye, nasi pia tutaweza kushiriki katika ahadi hizi. Kwakuwa kama tunamuhusu Kristo, nasi pia ni uzao wa Abrahamu. Tunasoma mstari wa mwisho kwa Wagalatia 3:

> *"Na ikiwa ninyi ni wa-Kristo, basi ninyi ni uzao wa Abrahamu, sawasawa na ahadi ya urithi."*

Mpaka hapo, nasi pia, tutashiriki ahadi. Tutapata uzima wa milele, na kumsaidia Yesu Kristo katika kazi kubwa ya kuleta furaha duniani. Tunaweza kuwa "uzao wa ABRAHAMU" (watoto) kwa kuamini na kubatizwa katika jina la Yesu Kristo. Hii ndiyo hasa ya kile anacho kisema Paulo kwa Wagalatia 3:27-29:

"Kwa maana nyote mmebatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani, hapana mtumwa wala mtu huru, hapana mtu mme wala mke: kwa maana nyote ni wamoja katika Kristo Yesu. Na ikiwa ninyi ni wa-Kristo basi ni uzao wa Abrahamu na warithi sawasawa na ahadi."

Utakumbuka kuwa moja ya ahadi ilikuwa,

> "Na kwa uzao wako mataifa yote ya dunia yatabarikiwa" (Mwanzo 22:18)

Ahadi hizi zitatimizwa wakati Yesu atakaporudi kuusimamisha Ufalme wa Mungu.

Ni vipi Abrahamu?

Lakini unaweza kufikiria, Ni vipi Abrahamu? Kamwe hakuzipokea ahadi, naye alikufa.

Hiyo ni kweli. Lakini ahadi za Mungu haziwezi kukosa kufanyika. Yesu akirudi tena atamfufua Abrahamu na Isaka toka wafu - na isitoshe wengi wengine - na wataishi milele duniani, wakifurahia baraka hizo ambazo Mungu aliziahidi zamani sana.

Utambue kwamba Mungu hakumwahidi Abrahamu sehemu ya ufalme juu mbinguni, bali aliahidi wa nchi aliyo iona na aliishi ndani yake.

Muhutasari

1. Abrahamu aliitwa na Mungu atoke Uru aende katika nchi asiyo ijua
2. Nchi hii ni nchi ya Israeli, na Mungu aliahidi kwamba ataimiliki milele.
3. Pia, Abrahamu aliahidiwa kupata mtoto; kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa, na kwamba mwanawe atakuwa baraka kwa mataifa yote.

masomo ya biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian.

Karatasi Ya Maswali Ya 4

Jaribu na ujibu maswali kwa maneno yako mwenyewe. Mahali panapotaja "kazi ya ziada" unaweza kujibu swali ukipenda, au kuliacha kama utaona ni gumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali mengine yote. Kumbuka kuandika namba yako, jina na anuani yako juu ya kila karatasi ya majibu yako.

MASOMO 12 - 15

12a Mungu alimwambia Ibrahimu afanye nini wakati Ibrahimu alipokuwa akiishi Uru?

12b Mungu alimwambia Ibrahimu amfanye nini Isaka?

12c Neno "uzao" linamaanisha nini (kama ilivyo katika Mwanzo 13:15) ?

12d Ni uzao upi ulio muhimu sana wa Ibrahimu?

12e Kwa sababu Ibrahimu alimwamini Mungu na kumtii, Mungu alimbariki. Kati ya baraka zote hizo mbalimbali, zipi 2 unafikiri ni muhimu zaidi? Sema ni kwa nini.

13a Andika mistari michache kuhusiana na kila mojawapo ya majina yafuatayo: (a) Yusufu; (b) Musa; (c) Sauli.

13b (a) Kwa nini Mungu aliwafanya watu wa Israeli wachukuliwe uhamishoni?
(b) Ni katika nchi gani watu wa Yuda walipelekwa uhamishioni?
(c) Walikaa huko kwa muda gani?
(d) Walifanya nini mara baada ya kurudi?

14a Ni mistari ipi katika Zekaria 14 inalenga kwenye yafuatayo:
(g) Mataifa yote yatakuja kupigana na Yerusalemu.
(h) Bwana atawapigania Israeli.
(i) Yesu Kristo atarudi katika mlima wa Mizeituni.
(j) Bwana atakuwa Mfalme juu ya nchi yote.
(k) Watu waliofanya vita juu ya Yerusalemu watapigwa na tauni.
(l) Watu watakaosalia (wa mataifa yote waliokuja kupigana na Israeli) watakwea kwenda Yerusalemu kumwabudu Mfalme.

14b Katika maneno yako mwenyewe, yasiyozidi mistari 10, elezea unabii juu ya mifupa mikavu unamaanisha nini.

Kitu kingine cha kutegemea

Paulo anatuambia katika Waebrania 11:39-40:

> *"Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; katika hili kwakuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."*

Sasa Abrahamu, na Daudi, na wengi wengineo watu waaminifu, walikufa wakijua kwamba katika siku ya kuja Yesu Kristo watafufuliwa tena na "kukamilishwa" - nakupewa uzima wa milele wote wanaomhusu Yesu. Lakini kama fungu la maneno linavyoonye aha, uzima wa milele hautakuwa kwa ajili ya watu waaminifu peke yao. Unawezakuwa kwa ajili yetu pia.

Mstari wa maana
Tume ona ya kwamba Yesu Kristo pande zote mbili ni wa uzao wa Abrahamu na wa uzao wa Daudi. Mstari wa kwanza kabisa wa Agano Jipya unaanza:

> *"Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu."*

Basi tunaweza kulielewa Agano Jipya, kama tumesoma na kulielewa Agano la Kale

Muhutasari

1. Mungu alimwahidi Daudi kupata mtoto.
2. Mtoto alikuwa ni Yesu, Mwana wa Mungu.
3. Atamiliki kiti cha enzi cha Daudi milele.
4. Atakapokuja kutawala, watumishi wote wa Mungu watapewa uzima wa milele, nao watashiriki kati1ca Ufalme duniani.

Sura za kusoma : 1 Samueli 17; 1 Mamboya Nyakati 17
Jifunze kwa moyo : 1 Mambo ya Nyakati 17: 11 , 12

> *"Hata itakuwa, siku zako zitakapo timia, uende na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayekuwa wa wana wako; nami nitaufanya imara ufalme wake. Yeye ndiye atakayenijengea mimi nyumba, nami nitakifanya kiti chake cha enzi cha ufalme wake."*

4. Abrahamu akapata mwana, Isaka, aliyezaliwa kwa muujiza wakati wazazi wake wakiwa wazee sana. Yesu Kristo pia ni mwanawe, au mzao, wa Abrahamu (naye pia alizaliwa na muujiza - kwa Bikira).
5. Ikiwa sisi tunamuhusu Kristo (kwa imani na kubatizwa), twahesabiwa kama watoto wa Abrahamu. na tutashiriki ahadi alizozifanya kwake.
6. Ahadi hizi zitatimizwa wakati Yesu akirudi, na kuuweka Ufalme wa Mungu.

Kidokezo

Yote haya kuhusu uzao wa Abrahamu kidogo ni vigumu kuelewa mara ya kwanza.
Lakini ni muhimu sana. Kwanini usisome sehemu hii hata mwisho mara nyingine tena - sana.
Sura za kusoma: Waebrania 11 (angalia hasa mistari 39-40)
Jifunze kwa moyo: Wagalatia 3:27-29

Orodha ya ahadi za Mungu kwa Abrahamu

Katika Kitabu cha Mwanzo	Kile Mungu alicho muahidi Abrahamu	Maelezo
12:2	Abrahamu atakuwa taifa kubwa	Abrahamu alikuwa ni Myahudi wa kwanza
12:2	Mungu atambariki	Toka mzao wa Abrahamu Yesu tunaweza kubarikiwa na wokovu
12:3	Kwa Abrahamu mataifa yote yatabarikiwa	na kuwa na sehemu katika ufalme wa Mungu dunia ni
12:7		Hii ilikuwa ni nchi yaIsrae
13:15	Nchi ambayo Abrahamu aliishi	
13:16	Wazao wa Abrahamu watakuwa kama mavumbi hesabu	Mbali ya majaribo ya kutaka kuwaangamiza, Wayahudi bado wapo kwa idadi kubwa leo

Pia angalia Mwanzo 15:6-8 22.16-18

MAFUNZO YA BIBLIA YA WAKRISTADELFIANI KWA NJIA YA POSTA Na. 13

WAIAJWDI KATIKA HISTORIA (Sehemu ya 1).

Somo: Mwanzo 37

Mwanzo wa kisa

Kisa cha wayahudi kwa hakika kinaanza na mtu yule mwaminifu Ibrahimu. Alikuwa na tote wa kiume aliyempata uzeeni aliyeitwa Isaka; Isaka alikuwa na mtoto wa kiume aliyeitwa Yakobo, ambaye baadaye alikuja. kuitwa Israeli. Yakobo alikuwa na watoto wa kiume kumi na mawili, ambao walikuwa ndio mababa wa yale makabila kumi na mawili ya Israeli.

Mtoto wa kiume wa pili. kutoka mwisho kati ya hao aliitwa Yusufu, na kisa cha maisha yake, kilichome kwenye Biblia, mara zote kinasisimua kukisoma. Lakini chenyewe ni zaidi ya kisa kizuri kinatueleza juu ya matukio muhimu katika. historia ya watu wa kwenye Biblia wayahudi. Kinatupa pia, mfano mzuri sana wa uangalizi wa Mungu uliokuwa ukibatilishwa juu ya watu wake.

Tunaweza kukumbuka masimulizi. juu ya kuuzwa kwa Yusufu kama mtumwa na ndugu zake wenye wivu; na jinsi, baada ya majaribu mengi, alivyokuja kuwa mtawala katika Misri. Kisha, wakati wa njaa, baba yak. na ndugu zake walifika Misri - shukurani kwa Yusufu, ma shukurani bila shaka, kwa Mungu -kulikuwepo nafaka nchini Misri.

Kwa muda, Wayahudi (pia wanaitwa Wana Israeli) walikuwa na furaha katika Misri. Lakini baada ya Yusufu kufa, idadi ya Wayahudi katika Misri ilipoongezeka zaidi na zaidi, Wamisri wakaanza kuwakandamiza, na kuwafanya watumwa.

Uhuru kwa watumwa

Pengine unakifahamu kisa cha jinsi Mungu alivyowatoa watu hawa wa Kiyahudi katika Misri, chini ya uongozi wa mtu aliyeitwa Musa, na akawaongoza kupitia nchi kame ma isiyokaliwa hadi kwenye kingo za nchi ya Israeli. Katika safari hii ndefu na ya hatari, Mungu aliwalisha na kuwaangalia. Kama tunavyosoma katika Nehemia 9:20-21:

> *"Ukawapa na roho yako mwema ili kuwaelimisha, wala hukuwanyima. mana vinywani mwao, tena ukawapa: maji kwa ajili ya kiu yao Naam, muda wa miaka arobaini uliwaruzuku jangwani, wasihitaji kitu; nguo zao hazikuchakaa, wala miguu yao haikvmba."*

Sheria iliyotolewa na Mungu

Walipokuwa wakisafiri kuiendea nchi waliyoahidwa na Mungu, walifika kwenye mlima Sinai. Pale kitu fulani maalumu kilitokea. Watu wale waliambiwa wajikusanye chini ya mlima, na hapa Mungu akawaambia:

> *"Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapekuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu" (Kutoka 19:5).*

Wale watu wakasema:

Mara nyingi Daudi aliitafakari ahadi hii ya heshima au agano, ambalo Mungu alifanya naye, na analizungumza agano hili katika Zaburi. Kwa mfano, Zaburi 89:2-4, tunasoma:

> *"Maana nimesema, Fadhili zitajengwa milele: katika mbingu utauthibitisha uaminifu wako. Nimefanya agano na mteule wangu, nimemwapia Daudi, mtumishi wangu , wazao wako nitawafanya imara milele, nitakijenga kiti chako cha enzi hata milele".*

AHADI ZA MUNGU KWA DAUDI (2 SAMUELI 7)

Fungu dogo la maneno	Maelezo mafupi
mstari wa 12: "Siku zako zitakapotimia nawe utakapolala na baba zako, nitainua mzao nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake.	Wakati maisha ya Daudi yamekoma na amekwisha kufa, Mungu atamwinua mmoja wa watoto wake, na Mungu atausimamisha ufalme wake.
mstari wa 13: "Ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu	Mtoto atajenga nyumba yake Mungu. (Sulemani alijenga nyumba ya Mungu. Yesu Kristo anajenga nyumba ya Mungu (tazama Waefeso 2:19-22.)
nami nitakiimarisha kiti chake cha enzi milele."	Mungu atakifanya kiti chake kiwe cha uhakika milele. (Sulemani hakutawala milele, Yesu atamiliki 'milele'.)
Mstari wa 14: "Nitakuwa Baba yake naye Mwana wangu.	Mungu atakuwa baba wa huyu mtoto wa Daudi, naye Mwana wa Mungu. (Yesu ni Mwana wa Mungu).
Kama akitenda uovu nitamwadhibu…"	Yesu hakufanya dhambi, hivyo Mungu hangemwadhibu.
mstari wa 16 "Nyumba yako na ufalme wako vitathibitishwa imara milele mbele yako:	Nyumba ya Daudi na ufalme vitasimamishwa, Daudi atakuwapo. (Mambo haya yatatokea Yesu akirudi na Daudi atafufuliwa na kuwapo katika ufalme.)
kiti chako cha enzi kitakuwa imara milele."	Wakati huo Yesu atakuwa anatawa1a toka kiti cha Daudi (yaani, kutoka Yerusalemu). Atatawala milele.

Mfalme wa Wayahudi

Yesu alizaliwa kuwa Mfalme. Mamajusi walipokuja kumsujudia, waliuliza:

"Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? (Mathayo 2:2).

Yesu alipokamatwa na kuletwa mbele ya Pilato kwa hukumu, Pilato alimuuliza:

"Wewe ndiwe Mfalme wa Wayahudi?" Yesu alijibu:

"Wewe wasema" (Marko 15:2).

Huo ni namna ya msemo wa Wayahudi, "Ndiyo, hakika ni mimi".
Kama tulivyoona, Yesu atarudi tena duniani kuwa Mfalme wa Wayahudi, na kutawa1a juu ya kiti cha enzi cha Daudi.

Ufalme utakaoenea pote

Yesu atakaporudi hatakuwa Mfalme wa Wayahudi pekee. Atatawala dunia yote.
Kwa habari zake Mungu anasema:

"Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia" (Isaya 49:6). ('Mataifa' maana yake watu wasio Wayahudi).

Vipi kuhusu Daudi?

Ingawa Daudi alitambua kuwa ahadi hii haitatimilika kwa muda mrefu sana, alijaa na shukrani kwa Mungu, nasi tunasoma sala yake ya shukrani katika 2 Samueli 7:18-29. Mungu alisema:

"Nyumba yako na ufalme wako vitathibitishwa milele mbele yako (yaani, utakapokuwepo)" (2 Samueli 7:16).

(Tambua: 'Nyumba' inaweza kumaanisha jengo-hekalu liliitwa nyumba ya Mungu lakini pia inaweza kuwa na maana jamaa (familia) au wazao.)Hiyo ndiyo maana
iliyo halisi katika ahadi zilizofanywa kwa Daudi.)

Basi Daudi alijua kwamba wakati hatimae Mtoto wake mkubwa (Bwana Yesu) akitawala kutoka Yerusalemu, yeye mwenyewe atafufuliwa toka wafu, ili kwamba aweze kufurahia raha ya kwenye ufalme.

"Hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda" (Kutoka. 19:8).

Kisha Mungu akampa Muss sheria zake, ma Musa akawapa wale watu. Bila shaka, zilikuwa ni sheria bora ambazo hakukuwa na taifa lingine lililokuwa nazo, na laiti tu Wayahudi wale wangezifuata, wangekuwa ni watu wenye furaha kuliko wote duniani.

Kama ishara kwamba wao wangekuwa watu wake, Mungu aliwaambia siku ya mwisho ya kila juma ingekuwa siku takatifu. Siku hii ingeitwa ‘Sabato’, na wangepaswa kupumzika na kutafakari juu ya wema wa Mungu kwao.

Lakini hawakuweza kuzifuata amri za Mungu. Hawakuweza kabisa kuzitii zote. Na hivyo ndivyo Mungu alijua ingetokea - kwamba wangejifunza kuwa wasingeweza kujiokoa wenyewe na kwamba walimhitaji Mungu awaokoe (hivyo ndivyo ilivyo kwetu pia). Hawakumtii Mungu mara nyringi tu, na hawakuifanya Sabato siku maalumu, kama alivyosema kuwa walipaswa kufanya hivyo.

Mwishowe walifika katika nchi ya Israeli. Mungu alikuwa mfalme wao. Aliwapa makuhani wa kuwafundisha njia zake, ma Waamuzi ili waamue juu yao.

Wayahudi wanataka mfalme

karibu miaka 400 ilipita. Wayahudi wakawa hawajaridhika na wakataka wawe na mfalme kama mataifa yaliyowazunguka. Kwa kutaka kwao mfalme, walikuwa wanakataa kutambua kuwa Mungu alikuwa ndiye mfalme wao Wakati Samweli, mwamuzi wao, alipomwambia Mungu jinsi walivyohitaji kuwa na mfalme, Mungu alisema:

"Hawakukukataa wawe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao" (1 Samweli 8:7).

Mungu aliwapa walichokitaka. ungependa kusoma mwenyewe kisa cha kuvutia cha kupakwa mafuta kwa Sauli, mfalme na kwanza we Israeli Utakikuta kisa hiki katika 1. Samweli 8 na: 9.

Ufalme uliogawanyika

Sauli alifuatiwa na Mfalme mkuu Daudi, ambaye utamsikia sana katika masomo yajayo. Baada ya utawala mrefu wa miaka 40, Daudi alikufa, na mtoto wake wa kiume, Sulemani akawa mfalme.

Sulemani alikuwa tajiri sana; aliwatoza watu kodi kubwa. Hali hii iliwafanya wanung‘unike. Sulemani alipokufa, wakamwendea mwanawe Rehoboamu, na kumwomba awapunguzie mzigo wao. Utaona katika 1 Wafalme 12, jinsi Rehoboamu alivyowasikiliza marafiki zake vijana, badala ya kufuata ushauri wa wazee waliokuwa na busara ambao walikuwa washauri wa baba yake.

Wakati wale watu walipomjia Mfalme Rehoboamu kutaka kujua iwapo angewakubalia ombi lao, aliwajibu bila chembe yoyote ya busara. Tunasoma katika 1 Wafame 12 kuwa mfalme "akawajibu wale watu kwa ukali", akisema,

> *"Baba yangu alilifanya zito kongwa lenu, bali mimi nitaongeza kongwa lenu; baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, bali mimi nitawapigeni wa nge (mstari 14).*

Haikuwa ajabu watu wale kumuasi mfalme kama huyo! Makabila kumi ya Israeli yakajitenga na kuondoka, na kuunda ufalme wao, chini ya mtu aliyeitwa Yeroboamu. Ni Yuda tu, kabila alilotoka Rehoboamu,. na lile dogo la Benyamini, ndiyo yaliyoendelea kumtii Rehoboamu.

Hivyo, kutoka wakati hue na kuendelea, tuna historia mbili, ziendazo sambamba, kwenye Biblia. Kuna ile historia ya yale makabila kumi, ambayo mara nyingi hutajwa kama ‘Israeli’ au Ufalme wa Kaskazini (kwa sababu yalikuwa upande wa kaskazini wa nchi) na ile historia ya yale makabila mawili yanayotajwa kama ‘Yuda’, am Ufalme wa Kusini

Uasi ulioendilea wa Wayahudi

Katika vitabu vyote viwili vya Vat alma tulisoma kisa cha kusikitisha cha jinsi watu wale walivyodumu katika kumsahau Mungu, na wakaziacha njia zake. mwishowe mambo yalikuwa mabaya zaidi mpaka Mungu akasema angewaadhibu watu wale, kama alivyowanya mara kwa mara kuwa angewaadhibu, kwa kuwafanya wachukuliwe.

Utumwani kutoka katika nchi yao. Utaona kutoka kwenye maneno haya ya 2 Nyakati 36:15-16 Jinsi Mungu alivyofanya kila alichoweza kuwarudisha watu wake kwenye njia zake:

> *"Naye Bwana, Mungu wa baba zao, akatuma kwao kwa mikono wajumbe wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu wake, na makeo yake; lakini waliwadhihaki wajumbe wa Mungu na kuyadharau maneno yake, na kuwacheka manabii wake, hata ilipozidi ghadhabu ya Bwana juu ya watu wake, hats kusiwe ma kuponya."*

Ujumbe wa Mungu kwa Daudi

Rudi tena kwa 2 Samueli, aura ya 7. Sehemu ya muhimu zaidi kwa ujumbe wa Mungu kwa Daudi ni mistari 12-16. Hapa Daudi anaahidiwa kuwa na mwana (tunapata tena neno hilo la Wayahudi 'mzao', ambalo maana yake ni mwana, au mtoto).

Anasema juu ya huyu mwana wa ahadi:

> *"Yeye ndiye atajenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele" (mstari wa 13).*

Jambo hili lilikuwa litokee baada ya kifo cha Daudi, maana ilikuwa iwe "hapo siku zako zikitimia" (mstari wa 12).

Zaidi kuhusu Mwana wa Daudi

Daudi alikuwa na mtoto alitawala Yerusalemu badala yake, jina lake aliitwa Sulemani. Kwa sehemu ahadi kwa Daudi zilitimizwa kwa Sulemani, lakini utimilifu kamili ilibidi usubiriwe mpaka kuja kwa Yesu Bwana. Sulemani alifanywa kuwa mfalme wakati Daudi angali hai. Na bila shaka, Sulemani hajatawala milele.

Mwana huyu wa ahadi ilimpasa awe ni mtu maalum kabisa, maana kwa habari zake Mungu anasema:

> *"Nitakuwa Baba yake, naye atakuwa ni Mwanangu" (2 Samueli 7: 14).*

Pungua Luka sura ya kwanza. Hapa tunasoma habari za malaika akija kwa Mwanamwali - mmoja wa watoto wa Mfalme Daudi, na kumwambia ya kuwa atapata mwana wa kiume. Huyu mtoto alikuwa azaliwe sio toka kwa baba wa kidunia, kama watoto wengine wanavyozaliwa, bali kwa njia ya uweza wa Mungu; kwa mwanamwali ambaye jina lake aliitwa Mariamu, aliambiwa;

> *"Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu Zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli: kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu" (Luka 1 :35).*

Vile vile malaika akamwambia Mariamu:

> *"Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu: na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo milele, nao ufalme wake hautakuwa na mwisho" (Luka 1:32-33).*

Sasa tunaona jinsi ahadi za Mungu kwa Daudi zilitimilika Yesu Kristo alipozaliwa.

1. Mungu alikuwa Baba yake.
2. Atatawala milele na milele.

Sura za kusoma: Ezekieli 36; Zekaria 14; Warumi 11
Mstari wa kujifunza: Zaburi 72:8

"Na awe na enzi toka bahari hata bahari, Toka mto hata mi ishe ya dunia."

KOZI YA BIBLIA YA KRISTADELFIANI KWA NJIA YA POSTA Na 15

AHADI ZA MUNGU KWA DAUDI

Somo: 2 Samueli 7

Kijana mchungaji aliyekujakuwa mfalme

Labda umewahi kumsikia Daudi kijana mchungaji aliyemuua Goliati mtu wa kutisha kwa jiwe moja kutoka kwenye kombeo.

Daudi aliishi miaka elfu nyuma kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo. Alizaliwa sehemu ile ile kama Yesu - kwenye mji mdogo uliokaribu na Yerusalemu unaoitwa Bethlehemu, naye alikuwa ni mtoto wa mwisho wa mchungaji wa wanyama aliyeitwa Yese.

Daudi alipokuwa ni bado kijana mdogo, Mungu alimtuma nabii Wake Samueli 111 kumpaka mafuta awe mfalme juu ya Israeli. Lakini wakati ule Mfalme wa kwanza aliyeitwa Sauli alikuwa anatawala. Sauli alikuwa ni mwenye wivu sana juu ya Daudi, na kwa nyakati kadhaa alijaribu kutaka kumuua, naye Daudi alikuja kuwa mkimbizi.

Sauli hakuwa ni mfalme mwema; alikuwa ni muasi kwa Mungu, ulifika wakati akauawa na Wafilisiti vitani.

Njia ikawa wazi kwa Daudi kuwa mfalme.

Baada ya mithihani mingi na mambo ya hatari, akajenga makao makuu Yerusalemu, hapo aliishi na kutawala.

Daudi alipowaza kuhusu namna alivyobarikiwa na Mungu, na kiisha kufikiri kuhusu Sanduku la Agano la Mungu ambalo bado lilikuwa linatunzwa ndani ya hema, akataka kujenga Hekalu zuri katika mji wa Yerusalemu ambamo Sanduku litahifadhiwa. (Sanduku la Agano lilikuwa ni kasha maalum ambalo ndani yake mlikuwa na Amri Kumi, na lilikuwa na mfuniko uliojulikana kama Kiti cha Rehema, juu yake utukufu wa Mungu uling'ara).

Daudi akamwambia Nathani, nabii wa Mungu, alichotaka kufanya. Nathani naye akamwambia Daudi aendelee; lakini usiku ule Mungu akanena na Nathani, kwa kumpa ujumbe mahususi wa Daudi.

Adhabu ilikuwa haina budi kuja

Ufalme wa Israeli Unagawanyika
UFALME ULIOUNGANA

Ufalme wa kaskazini wa Israeli	Ufalme wa Kusini wa Yuda
(MAKABILA 10)	(MAKABILA 2)
CHINI YA YEROBOAMU	CHINI YA REHOBOAMU
WAFALME WENGINE	WAFALME WENGINE
WALITEKWA NA KUTAWANYWA	WALICHUKULIWA UHAMISHONI
NA WAASHURI	KATIKA BABELI
HAWAKURUDI	WALIRUDI MIAKA 70

BAADAYE

Kutotii kama huko kulipaswa kuadhibiwe. Israeli, Ufalme wa Kaskazini, ulikuwa wa kwanza kuchukuliwa uhamishoni Mfalme we Ashuru alikuja ma. kuwachukua watu wale hadi Ashuru, na kama taifa, hawakuweza kurudi tena katika nchi yao.

Baadaye, Ufalme wa Yuda ukachukuliwa. uhamishoni na at sine we Babeli. Lakini Mungu aliahidi kuwa, baada ya miaka 70, wangerudi tens kwenye nchi yao wenyewe. Na wengi walirudi. Wakiwa wametiwa nguvu na manabii, walilijenga upya hekalu la Mungu Yerusalemu. Vitabu vitatu vya mwisho vya Agano la Kale - Hagai, Zakaria na Malaki - viliandikwa katika siku hizo.

Kipindi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya

Baada ya manabii hawa watatu, kulikuwepo muda mrefu — miaka 400 - ambapo Wayahudi hawakupata ujumbe we moja Iwa moja kutoka kwa Mungu. Nabii Amosi alikuwa ameonyeshwa kuwa kipindi hiki kingetokea. Katika Amosi 8:11 tunasoma:

"Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya Bwana."

Kipindi hiki cha miaka 400 kinaangukia kati ya kitabu cha mwisho cha Agano la Kale na kitabu cha kwanza cha Agano Jipya. Sio ajabu kwamba Yohana Mbatizaji alipotokea kulikuwepo maisimko mkubwa miongoni mwa watu. Baada ya mamia ya miaka ya ukimya, Mungu alikuwa amezungumza tena kwa watu wake.

Myahudi mkuu

Yohana Mbatizaji alitumwa ma Mungu kuandaa njia kwa ajili ya mtu mwingine mkuu zaidi. Mungu alikuwa anakaribia kumtuma mwanawe ili awaokoe watu wake. Na hivyo, katika nchi ya Israeli, karibu miaka 2000 iliyopita, Bwana Yesu Kristo alizaliwa. Mara nyingine huwa tunasahau kuwa Yesu alikuwa Myahudi.

Unaelewa kilichotokea. Baada ya kuyasikia maneno yake, ma kuyaona maajabu aliyoyatenda, Wayahudi walimkataa Yesu. Walimshawishi Pilato amsulubishe. Pilate aliposema, "Mimi sins sine hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki," Wayahudi wakajibu, "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu"
(Mathayo 27:24-25),

Wasingeweza kutenda kosa bays zaidi ya hili. Walimwaga damu isiyokuwa ma hatia ye Mwana wa Mungu. Lakini, kwa mahubiri ya nguvu yy mitume, Mungu aliwapa tena nafasi nyingine. Wayahudi wengi hawakukubali kuipokea rehema ya Mungu, na adhabu ilibidi ije. Adhabu ya kuogofya kabisa!

Watu wasio na makazi

Karibu miaka arobaini baada ya kifo cha Yesu, jeshi is Warumi lilikuja ma kupigana na Wayahudi. Kilikuwa ni kipindi cha mateso makubwa. Maafa ya vita hiyo ni baadhi ye maafa ye kutisha mno katika historia ye mwanadamu Mji ulichukuliwa na Warumi, na Wayahudi wale walionusurika walitawanywa huko ma huko miongoni mwa mataifa ye dunia.

Mungu alikuwa amewaonya Wayahudi tangu zamani kuwa hili lingetokea iwapo wangeziacha njia zake. Utasoma katika Kumbukumbu la Torati 28:64:

> *"Bwana atakutawanya katika mataifa yote, tokea ncha hii ya dunia hata ncha hii ya dunia."*

Na hivyo, kwa karibu miaka 2,000, Wayahudi hawakuwa na nchi yao wenyewe. Kibaya zaidi ye hiki, wameteswa na kunyanyaswa sana, na laana ya kuogofya katika Kumbukumbu la Torati Sura ya 28 imewashukia. Baadhi ya udhalimu waliotendewa umetukia katika vipindi vya karibuni kabisa. Wengi wetu tunaweza kukumbuka makambi ya mateka ye Hitler wakati wa Vita kuu ya Dunia ya 1939-45. Zaidi ye Wayahudi milioni sita waliuawa kwa ukatili ambao uliutikisa ulimwengu. Soma tena Kumbukumbu la Torati 28:64~67, na Utastaajabu kwamba maneno haya, yaliyoandikwa na Musa zaidi ya miaka 3,000 iliyopita, yamekuja kutokea katika nyakati zetu.

Ni kisa cha kuhuzunisha, lakini bado hakijamalizika. Tunapaswa kufurahi tunaposoma kutoka katika neno la Mungu kwamba mwisho wa kisa hiki utakuwa we furaha,

Usisahau kuwa Ufalme huo sio wa Wana Israeli tu. Watu wa Mataifa (wasiokuwa Wayahudi) wanaweza kupata nafasi katika Ufalme huo kwa neema ya Mungu, iwapo
Mtume Paulo alipekuwa akiwaandikia Warumi, waliokuwa watu wa Matafia alitumia mfano wa mti wa mzeituni kuonyesha kuwa watu wa Mataifa wanaweza kujiunga na kile kilichoahidiwa kwa Wayahudi.

Jisomee mwenyewe kuhusu habari hii katika Warumi 11 (hasa mstari wa 13 hadi wa 25) na angalia maonyo na tahadhari anazotoa!

WAYAHUDI NA WATU WA MATAIFA KATIKA MPANGO WA MUNGU - WARUMI 11

<table>
<tr>
<td> 
Israeli ikiwakilishwa na mti wa mzeituni</td>
<td>
Baadhi ya mtatawi yanaondolewa. Matawi haya yaliyoondolewa yanawaki Wana Israeli ambao hawamwamini Mungu (mstari wa 17—20)</td>
</tr>
<tr>
<td> 
Matawi kutoka kwenye mzeituni mwitu yanawaza kupandikizwa kwenye shina. Haya yanawakilisha Mataifa watakaoamini na hlvyo kuun anishwa kwenye Ufalme</td>
<td> 
Baadhi ya matawi ya mwanzo yanaweza kupandikizwa tena kwenye shina Mungu anawaza kuwakaribisha tena Wayahudi watakaomgeukia tena na kumwamini (mstari 23)</td>
</tr>
</table>

Mstari unaofuata unaonyesha jinsi Mungu atakavyewasaidia atamtuma tena Yesu!

"Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni. . ."

Hebu fikiria jinsi Wayahudi watakavyojisikia watakapong'amma nini kimetokea. Yesu Kristo, waliyemsulubisha, amerudi kutoka mbinguni, na amewaokoa Mwishowe watamtambua na kumkubali. Ni nabii Zekaria ambaye anatuambia tena:

"....nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee" (12:10).

Hatua ya 1	Israeli wanatawanywa na kuadhibiwa kwa uovu wao	Ezekieli 36: 16-20
Hatua ya 2	Mungu anawakusanya tena Israeli	Ezekieli 36:21-24
Hatua ya 3	Israeli wanabadilishwa	Ezekeli 36:25-28

Kuusimika tena Ufalme wa. Mungu duniani

Baada ya Wayahudi kuwa wametubu, Yesu atatawala kutoka Yerusalemu. Wakati Yesu atakapokuwa mfalme na sheria za Mungu Kuwapo duniani, dunia itabadilika na kuwa tofauti. Lakini ni vipi kipindi hiki cha amani duniani kitakavyeletwa?

Katika historia nzima ya mwanadamu, matafia yamekuwa yakifuata njia zao. Wamej ifurahisha nafsi zao na kumpuuza Mungu Bado wanafanya hivyo! Wakati Bwana Yesu Kristo atakapokuwa amesimikwa Yerusalemu, atayaamrisha mataifa yote "kumcha Mungu, na kumtukuza" (kama Ufunuo 14:7 inavyosema). Mataifa yale yatakayomkubali Bwana yatabarikiwa mno katika Ufalme wake.

Lakini Bwana Yesu Kristo atakuwa na uwezo wa kuliadhibu taifa lolete ambalo litamwasi. Zekaria sura ya 14 inatuambia kwamba taifa lolote ambalo litakataa kwenda Yerusalemu kuabudu mara moja kwa mwaka mvua haitanyesha kwao. Na iwapo taifa, kama Misri ambale kwa kawaida hupata mvua kidogo sana, litakapoketaa kutii, litatafunwa na tauni.

Hivyo utakuwa ni wakati wa. amani na furaha. kwa dunia nzima. Kuna vielelezo vingi vizuri vya kipindi hicho kwenye Biblia. Kimoja kati ya vielelezo hivyo kinapatikana kwenye Isaya 11:6,9:

"Mbwa mwitu atakaa pamoja na mwanakondoo, na chui atalala pamoja na mwanambuzi; na mtoto mdogo atawaongoza... Hawa tadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari."

Jedwali hili linweza kukusaidia(miaka imekadiriwa)

1. Miaka 3,500 iliyopita	Mungu aliwatoa Wayahudi Misri, na akawapa nchi ya Israeli waishi humo. aliwafundisha njia zake. Badala ya kuwaonyesha watu wa Mataifa waliowazunguka jinsi Mungu alivyowataka waishi wakawaiga watu hao waovu we Mataifa.
2. Miaka 2,500 iliyopita	Mungu hatimaye aliwaadhibu kwa kuwapeleka uhamishoni. Ufalme wa Kusini wa Yuda ulirudishwa katika Israeli baada ya miaka 70, lakini bado wakaendelea kutomtii Mungu.
3. Miaka 2,000 iliyopita	Baada ya kusulubiwa kwa Yesu, Wayahudi waliondolewa katika nchi yao. Kwa karibu miaka 2,000, wamekuwa watu wasio na kwao na wakifanyiwa udhalimu.
4. Leo	Mungu anawarudisha katika nchi ya Israeli. (Utasikia mengi kuhusu hili katika somo lijalo)

Sura za kusoma: Kumbukumbu. la Torati 28; 2 Mambo ye Nyakati 36:11-23
Jifunze moyoni: Isaya 43:11,12

MAFUNZO YA BIBLIA YA WAKRISTADELFIANI KWA NJIA YA POSTA
Na 14
WAYAHUDI KATIKA HISTORIA (Sehemu ya 2)
Somo: Ezekeli 37

Bonde la Mifupa Mikavu
Ezekieli alipewa maono ya ajabu. Yameandikwa katika Ezekieli sura ya 37. Kuna hatua tatu tofauti.

1. Ezekieli aliona bonde lililokuwa wazi likiwa limejaa mifupa mikavu sana.

2. Ezekieli alitakiwa kuitolea unabii mifupa ile, na kwa kishinde kikuu, mifupa ikasegeleana, mpaka vikawapo viwiliwili vingi vya mifupa vilivyokamilika. Ezekieli alipondelea kutazama, mifupa ikafunikwa na mishipa, nyama na ngozi juu yake. Lakini bado haikuwa miili hai.

3. Mungu sasa alimwambia Ezekieli autabirie upepo ili kwamba miili hiyo ijazwe pumzi, Ezekieli akafanya hivyo, na pumzi ilipoingia miili hiyo, ikasimama na ikawa JESHI KUBWA MNO!

Kwa hiyo inaongelea nini habari yoe hii? Ezekieli aliambiwa:

"Mwanadamu, mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli; tazama wao husema mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yamepotea; tumekatiliwa mbali kabisa" (Ezekieli 37:11).

Hivyo Hatua ya 1:	Mifupa Mikavu	INAMAANISHA	Israeli isiyo na tumaini (walitawanywa kote duniani na kuteswa)

Mungu anaendelea kusema katika mstari wa 12:

"Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli."

Hivyo, Hatua ya 2:	Mifupa inaunganika pamoja na kupewa miili	INAMAANISHA INAMAANISHA	Mungu anawarudisha nchini Israeli watu wake waliotawanyika

Mwisho, kuhusu kupewa kwao pumzi, Mungu alisema (mstari wa 14):

"Nami nitatia roho yangu ndani yenu, nanyi mtaishi, nami nitawawekeni katika nchi yenu, nanyi mtajua ya kuwa mimi Bwana, nimesema hayo, na kuyatimiza."

Hivyo, Hatua ya 3:	Miili isiyokuwa na uhai inapewa pumzi	INAMAANISHA	Mungu anatea roho yake kwa Israeli ili kwamba waelewe kuwa yeye ndiye mweza wa

Hatua ya 1

Hii tayari imekwishatimia. Israeli wametanywa na wake katika kukata tamaa, wakiutimiza unabii kama ule wa Kumbukumbu la Torati 28:65-67:

"Wala katika mataifa hayo hutapata raha iwayo yote, wala hutakuwa na kituo cha wayo wa mguu wako; lakini Bwana atakupa huko moyo wa kutetema, na macho ya kuzimia, na roho ya kudhoofika; na. uzima wako utakuwa wa wasiwasi mbele yake; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutaamini kamwe maisha yako; asubuhi utasema, Laiti ingekuwa jioni! na jioni utasema, Laiti ingekuwa asubuhi! kwa kicho cha moyo wako utakavyokucha na kuona kwa macho yako utakavyoona."

Hatua ya 2.

Imekuwa ni hivi karibuni ambapo watu wa Israeli wamekuwa wakirudi kwenye nchi yao. Mwaka 1917. Azimio la Balfour lilitiwa saini. Hili lilikuwa ni ahadi kwamba Waingereza wangeifanya nchi ya Palestina (sasa inaitwa Israeli) kuwa nchi ya. taifa la Wayahudi.

Wakati Hitler alipoingia madarakani jerumani aliazimia kuwaangamiza Wayahudi na zaidi ya Wayahudi milioni sita waliuawa katika mazingira ya. kutisha. Kwa sababu ya kuteswa kwao walijawa na hamu ya kurudi Israeli na kuwa na nchi ya kwao wenyewe ambako wangekuwa huru kutokana na udhalimu.

Mwaka 1948, baada ya vita kali, Israeli ilijitangaza kuwa taifa, Licha ya matukio hayo yasiyo ya. kawaida, Israeli imenusurika kama taifa. Kwa nini? Mungu a1isema: wangenusurika — kumbuka mstari wa: 12 wa Ezekieli 37!

Pia Yeremia alitabiri haya:

Maana mimi ni pamoja nawe, asema Bwana, nikuokoe; maana nitawakomesha kabisa mataifa yote huko niliikowatawanya, bali sitakukomesha..." (Yeremia 30:11)	Aliyemtawanya Israeli atamkusanya, na kumlinda, kama mchungaji alindavyo kundi lake. Kwa maana Bwana atamweka huru Yakobo, amemkomboa mkononi mwake aliyekuwa hodari kuliko yeye (Yer. 31:10-11)

Hivyo hatua ya 2 inatimia sasa, karne hii! !

Vipi Kuhusu i1e hatua ya tatu?

Je, taifa la Israeli linatambua kwamba Mungu ndiye mtawala? Kwa masikitike, hapana, halitambui. Wakati utafika, hata hivyo, ambapo Israeli atabadilishwa moyo wake. Zekaria 14 inatuonyesha kwa nini itakuwa hivyo! Soma mstari wai hadi wa 4.

Wakati umakuja ambapo mataifa yatajikusanya dhidi ya Israeli. Kutokana na mambo yanayotekea ulimwenguni sasa, wakati huo hauko mbali kutoka sasa.

Pale ambapo kila aina ya tumaini litakapokuwa limepotea kwa Israeli jambo la kutia moyo litatukia.

Zekaria 14: 5 inasema:

"Hapo ndipe atakapotekea Bwana, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipepigana zamani siku ya vita."